East African Journal of Swahili Studies, Volume 7, Issue 1, 2024
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 7, Issue 1, 2024
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

# Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya

*Dkt. Alexander Rotich, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030 - 20200 Kericho, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: arotich@kabianga.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*13 Februari 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Skaz, COVID-19, Mtazamo, Kizuizui, Kericho.*

## IKISIRI

Madhumni ya makala haya yalikuwa ni kubainisha na kuchanganua mitazamo ya WaKenya kuhusu Tangaavu la Korona (COVID-19) kama inavyodhihirika kupitia mazungumzo ya kikawaida, Skaz. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, tafiti za awali kuhusu mada hii hazikukitwa katika misingi ya Skaz. Kwa hivyo, taarifa nyingi kuhusu Tangaavu la Korona zilizowasilishwa na Shirika la Afya Ulimwenguni pamoja na Wizara ya Afya nchini Kenya zilikuwa za kitaalamu (kiakademia). Utafiti huu ulikuwa wa nyanjani na ulifanyika Kericho, Kenya. Mtafiti aliteua sampuli kimakusudi na kukusanya data kwa kutumia mbinu ya utazamaji nyanjani. Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya Usemezano ikijumuisha sifa za Skaz kama ilivyoelezwa na Bakhtin ikitiliwa nguvu na Mbinu ya Urazini wa Kiwatu kama ilivyoendelezwa na Sacks na wenzake. Uchanganuzi wa data ulionesha kuwa, mwanzomwanzo, kutokana na kukosa ufahamu wa kitaaluma kuhusu ugonjwa "mpya" Tangaavu la COVID-19 kwa jumla, bila kukusudia kupotosha WaKenya waliibuka na mitazamo mbalimbali kuhusu ugonjwa huu. Mitazamo hii pia ilitokana na jitihada za hekaheka kutafuta njia za kuzuia usambazaji na hata tiba miongoni mwa wanajamii. Utafiti huu umeweka wazi mitazamo "hasi" kuhusu ugonjwa wa COVID-19 jinsi ili(na)vyodhihirika katika mazungumzo ya kikawaida na hivyo kuwafaidi watafiti wa utabibu na wapangaji sera za kiserikali kutilia maanani mitazamo katika lugha ya kikawaida haswa kwenye majanga ya kiulimwengu.

**APA CITATION**

Rotich, A. (2024). Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 79-86. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754.

**CHICAGO CITATION**

Rotich, Alexander. 2024. "Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 79-86. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754.

**HARVARD CITATION**

Rotich, A. (2024) "Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 79-86. doi: 10.37284/jammk.7.1.1754.

**IEEE CITATION**

A. Rotich "Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 79-86, Feb. 2024.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

**MLA CITATION**

Rotich, Alexander. "Mitazamo ya Kiskaz Kuhusu Covid-19 Inavyojitokeza katika Lugha ya Wananchi Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Feb. 2024, pp. 79-86, doi:10.37284/jammk.7.1.1754.

## UTANGULIZI

Tangu kuzuka kwa janga la COVID-19 katika mji wa Wuhan nchini Uchina mwaka wa 2019, ugonjwa huu ulienea kote ulimwenguni na kusababisha madhara mengi na makubwa katika mataifa yote ulimwenguni. Kutokana na janga hili, mamilioni ya watu walipoteza maisha yao, wengine wengi kupoteza mali na ajira, biashara nyingi kuporomoka, na kuvurugika kwa utaratibu wa maisha uliozoeleka (Reliefweb, 2020). Ukweli ni kwamba walimwengu walijikuta katika hali ya kukumbwa na namna ngeni ya maisha, hali iliyosababishwa na mikakati iliyowekwa na serikali na taasisi za afya katika mataifa ya ulimwengu ili kudhibiti janga hili (Mghenyi, 2020b).

Serikali za mataifa ya ulimwengu zikishirikiana na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) katika jitihada za kukabiliana na janga hili. Ziliweka mikakati mingi ili kuzuia kusambaa kwa ugonjwa huu. Baadhi ya mikakati ambayo pia ni sheria (fatwa) za kufwatwa bila udhuru wowote ni pamoja na: kunawa na kutakasa mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni; kuvaa kizuizui kila wakati mtu anapokuwa hadharani; kuzingatia umbali wa takribani mita moja unusu kati ya mtu na mtu mwenzake; kutosalimiana kwa mikono; kutobusiana; kuepuka mikutano ya hadhara; na kufungwa kabisa mipaka ya matembezi kimaeneo na kiwakati. Nchini Kenya, serikali pamoja na kuweka mikakati hii, aidha ilipania kutoa maelezo kuhusiana na ugonjwa huu kila siku. Kupitia kwa Wizara ya Afya, serikali ilianza utaratibu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu ugonjwa huu; namna unavyoambukiza, la kufanya mtu anaposhuku kuambukizwa ili kuzuia kuenea kwake (Ministry of Health, 2020). Makala haya yanadhamiria kuangazia mwonoulimwengu wa watu wa kawaida mashinani wanavyofikiri kuhusu haliya zinazotokea katika jamii. Namna fikira zao zinavyoathiri maoni yao na namna zinawafanya wachangamkie haliya hizo. Kupitia kauli za kikawaida za watu wasiojali sheria za unenaji tulichanganua usemaji huo na kupata ina athari kubwa katika upitishaji wa sheria za kuchunga maisha ya wananchi seuze wakati wa janga la kiafya kama COVID-19.

## MAPITIO

Katika sehemu hii tumeweza kutoa maelezo ya skaz na sifa zake ili tupate kuelewa dhana hii inavyojitokeza katika usemaji wa watu wa kawaida ambao ndiyo umma mkubwa wa ulimwengu. Hali kadhalika, tumeweza kufafanua namna machapisho ya ripoti za kiserikali na za mashirika yasiyo ya kiserikali yalivyotambulisha janga hilo la COVID-19 kwa jumuiya nzima ya ulimwengu.

### Fasili ya Skaz na Sifa Zake

Kulingana na Schmid Wolf (2003), Skaz ni neno la Kirusi linalomaanisha "kusema, kuambia". Ni aina maalumu ya usimulizi unaohusishwa na fasihi ya Kirusi tangu mwaka wa 1830. Hata hivyo, usimulizi wa Skaz hudhihirika katika fasihi zingine za ulimwengu. Kimsingi, Skaz huhusisha msimulizi ambaye ni mtu wa kawaida asiyezuiliwa na uwezo wa kirazini na umilisi wa kiisimu anapowazungumzia wasikilizaji katika muktadha wake wa kijamii. Ni masimulizi yenye kuingiliwa na sauti nyingi; masemezano baina ya wanaozungumza; masimulizi yasiyopangwa—yanatokea papo kwa papo (Bakhtin, 1981). Isitoshe, yanachanganya lugha ya kimtaani na huonesha upekee na umahiri wa msimulizi na wala siyo mwandishi. Alakulihali, ni lugha ya watu wa kawaida, makabwela.

Lugha hii ya kikawaida huonesha kauli ghafi zinazotumika katika jamii ambazo hazina pingamizi za kimaongezi (Schmid, 2003). Kila mnenaji hujikuta mshiriki na hujionesha kwa lugha yake ya kipekee. Husema analolitaka na mitindo yenye kupambanua urazini wake. Jamii yenyewe ikakubali lugha ya aina hii na kuipa umuhimu. Huku kujisemea na kukubalika katika jamii ndiko kuliwafanya wataalamu wakereke

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

(WHO, 2020) kwamba mambo yafanywa kinyume na matakwa yao. Kauli yetu ni kwamba wataalamu hawakuelewa asili ya aina hii ya lugha ndiposa umuhimu wa kutafitiwa kwake na makala haya.

**Ripoti za Korona**

Baada ya kisa cha kwanza cha Korona kuripotiwa nchini Kenya Machi 2020, baadhi ya wanajamii waliibuka na mitazamo anuwai kuhusu ugonjwa huu. Baadhi ya mitazamo hiyo iliripotiwa na taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Afya Ulimwenguni na Wizara ya Afya ya Kenya. Aidha ripoti nyingine ziliwasilishwa magazetini na tafiti zilizofanywa wakati huo. Mathalan, Wizara ya Afya (2020) iliripoti kuwepo kwa mitazamo "hasi" na "potofu" miongoni mwa wanajamii (Mghenyi, 2020a). Baadhi ya mitazamo hiyo ilikuwa pamoja na kwamba: virusi vya COVID-19 ni zana ya kibayolojia iliyotengenezwa kimakusudi maabarani na kuachiliwa kwa jamii, uagizaji wa bidhaa kutoka mataifa yaliyoripoti uwepo wa COVID-19 ungesambaza virusi vyake, mtu angeweza kuambukizwa kupitia kwa wanyama wanaofugwa nyumbani, kunywa pombe kutazuia usiambukizwe COVID-19, COVID-19 huwaathiri wazee pekee yao, na kadhalika.

Shirika la Afya Ulimwenguni, WHO (2020) nalo liliripoti na kuisahihisha mitazamo "hasi" na "potofu" kadhaa kama vile: uogeleaji katika vidimbwi vya kuogelea vya umma huambukiza COVID-19, kuvaa kizuizui kwa muda mrefu humkosesha mtu oksijeni, kuongeza pilipili kwenye supu na vyakula vingine hutibu COVID-19, hali joto ya baridi na barafu huua virusi vya COVID-19, mbu huambukiza COVID-19, na kadhalika.

Kwa upande wa ripoti magazetini, AFP (2021) katika gazeti la *The Standard*, anazungumzia mitazamo "hasi" miongoni mwa wanajamii kuhusu COVID-19. Baadhi ya mitazamo hiyo ni pamoja na kuwa; chanjo hubadilisha muundo wa DNA ya mtu, baridi kali huua virusi vya Korona, kizuizui iliyotengenezwa kwa kitambaa haizuii kuenea kwa virusi vya COVID-19, kunywa maji kwa wingi kutatoa virusi nje ya mwili na kuepuka kwenda hospitalini ili mtu adumishe afya yake. Isitoshe, mitazamo mingine hasi ni kama vile; dawa za ARV na zile za malaria hutibu COVID-19, vinywaji moto na vileo vinaweza kukomesha COVID-19 (Vidija, 2021).

Ripoti nyingine inayohusu mitazamo "hasi" kuhusu tangaavu la COVID-19 inatoka kwenye Kaunti ya Turkana. Ripoti hii inahusu fikra za watu wakiwemo hata wataalamu madaktari kuhusu COVID-19 katika Kaunti ya Turkana, kaunti yenye joto jingi. Mwandishi wa ripoti hii anasema kwamba, watu wengine hufikiria virusi vya COVID-19 haviwezi kusitawi kwenye halijoto jingi, hivyo wakaazi wa maeneo yenye joto kali kama WaTurkana hawawezi kuambukizwa. Mathalan, mmoja wa wakaazi aliyehojiwa na mwandishi alikuwa na haya ya kusema; "*Tunasikia kuwepo kwa Korona huko Nairobi lakini sio hapa, hapa tuko na njaa na malaria miongoni mwa watu wazima na watoto, hata mbuzi wetu wana magonjwa yao na hivyo ndivyo tunavyochukulia Korona*". Katika ripoti hii pia, daktari mmoja, mhudumu katika Hospitali ya Rufaa ya Lodwar alisema; "*Awali tulikuwa na fikra kwamba Korona haikuwepo katika Kaunti ya Turkana kwa sababu ni sehemu ya joto jingi na hivyo mtu hangeambukizwa. Lakini sasa fikra hiyo ilibatilishwa tulipoanza kuwapokea watu waliokuwa wameambukizwa*" (CGTN, 2020)

Kilonzo na Omwalo (2020) wakiwarejelea Ozili na Arun (2020), wanasema kuwa, kukosekana kwa ufahamu kuhusu jinsi virusi vya COVID-19 huambukizwa na namna uambukizaji huu ungesitishwa kuliwafanya watu watafute njia za kukimbilia usalama. Hali hii ngeni ya maisha iliwafanya waibuke na mitazamo ya kuieleza hali yenyewe. Kulingana na watafiti hawa, baadhi ya mitazamo ilikuwa pamoja na; kibayolojia, mwili wa mwafrika una kinga dhidi ya virusi kama vya COVID-19. Ithibati waliotoa ni maafa machache yaliyoshuhudiwa barani Afrika ikilinganishwa na mabara mengine. Pia, kulikuwa na fikra kwamba, hali ya joto barani Afrika haingewezesha virusi vya Korona kusitawi. Isitoshe, ilisemekana kuwa, vyakula vya kiasili vya kiafrika vina uwezo wa kuimarisha kinga dhidi ya virusi vya Korona.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

Mtazamo mwingine "hasi" uliobainishwa na kuwasilishwa na watafiti hawa ni kuwa, maombi ni kinga dhidi ya COVID-19. Wanaeleza kuwa, raisi wa nchi moja ya Afrika Mashariki alidai hakukuwa na COVID-19 nchini mwake kwa sababu ya maombi. Kiongozi huyo alikuwa akimtaja Mungu kila mara katika hotuba zake za kampeini dhidi ya COVID-19 (BBC, 2020)

Ripoti zilizowasilishwa hapo juu zilihusu maelezo "hasi" na "potofu" ya waathiriwa wa COVID-19 kwa sababu ziliangaliwa kitaaluma na kisheria ya kiserikali ili kudhibiti hali mbaya isienee. Walakini, wananchi wa kawaida mitaani na vijijini waliendelea kukiuka fatwa hizo. Utafiti wetu unapendekeza kuwa hali ilidororeshwa kwa sababu mwonoulimwengu wa wananchi wa kawaida haukutiliwa maanani na wataalamu hawa wakati wa kuweka sera zao za udhubiti wa janga hilo.

## MSINGI WA NADHARIA

Skaz ambayo ni lugha ya watu ambao hujizungumzia kutokana na mwonoulimwengu wao na husakini katika maongezi yao kuwa ni stahikifu na hakika kama inavyojitokeza katika Usemezano, nadharia iliyoasisiwa na Bakhtin (1981) na Mbinu ya Urazini wa Kiwatu iliyoitifakiwa na Sacks na wenzake (1974) ndiyo dhana iliyoongoza utafiti wetu. Ripoti kadhaa tulizotaja hapo juu zilichukulia kuwa ni 'upotoshaji' unaoelekea kwenye udanganyifu lakini utafiti huu unajadili na kupendekeza kuwa, katika lugha ya kikawaida masemezano hayo ya wananchi wa tabaka la chini ndiyo ukweli wa kihakika kwa sababu ya imani ya mwonoulimwengu wao hivyo kuna haja ya kuangalia upya maana ya 'upotoshaji' huo kwa faida ya majanga yajayo.

Utafiti huu utachukulia kuwa maelezo ya kitaaluma kuhusu Tangaavu la COVID-19 ndicho mame-aina cha kuakisia utofauti wa maono ya wananchi kuhusu ugonjwa huo. Kwa sababu ya ujuzi wao wa kitaalamu, matabibu, na watafiti waliaminiwa zaidi na wapanga sera za serikali hivyo kauli yao ni aminifu na stahikifu. Kwa mintarafu ya mame-aina hicho tuliangalia namna wananchi walivyotoa maelezo yao ya kiSkaz na ambayo kwamba yaliwakera wataalamu na mashirika ya kiulimwengu hadi kutunga Maswali Yanayoulizwa Sana (FAQs) kuhusu ugonjwa huu, hatua ambayo ilichukuliwa kudhibiti aina yoyote ya 'upotoshaji' (Ministry of Health, 2020).

## MBINU ZA UTAFITI

Ukusanyaji wa data ulifanywa mjini Kericho katika Agosti ya 2020, miongoni mwa wafanyabiashara sokoni. Mji wa Kericho ni mji mkubwa wenye masoko ya wazi yaliyotapakaa mji mzima na pembezoni mwake. Tulitembelea masoko ya: Soko Kuu, Jua Kali, Nyagacho, Majengo na Kapsuser. Watafitiwa walioteuliwa kupitia kwa usampuli kimakusudi waliulizwa maswali ana kwa ana. Kwa ujumla wasailiwa 20 (5 kutoka kila soko) waliteuliwa kwa sababu mtafiti angewafikia kwa urahisi na kutagusana nao kwa wepesi. Tunaamini kuwa sampuli hii ni kiwakilishi toshelezi cha jumuia nzima ya Kenya kwa sababu iliripotiwa mitazamo ya aina hii ilishuhudiwa kwingineko (CGTN, 2020). Aidha mbinu ya kushiriki kusikiliza mazungumzo ya kawaida ya watafitiwa ilitumiwa. Mazungumzo haya yalinukuliwa kimaandishi kisha kuchambuliwa. Ingawa wanajamii wanaweza kuwa na mitazamo chanya na vile vile mitazamo hasi, mtafiti alijifunga katika kuchanganua mitazamo "hasi" pekee. Mchakato huu mzima uliongozwa na sifa za usimulizi za Skaz.

## MATOKEO

Baada ya uchanganuzi wa data tuliweza kubainisha mitazamo mbalimbali inayojitokeza katika lugha ya Skaz. Mitazamo yenyewe ilihusu dhana ya ugonjwa wa Coid-19, imani juu ya tangaavu hilo, ugonjwa unavyoambukizwa, unaowaambukiza, dalili zake na matibabu yake.

### Mitazamo Kuhusu Ugonjwa Wenyewe na Usambazaji Wake

Kutokana na maongezi ya kikawaida, ilidhihirika kwamba, baadhi ya WaKenya walikuwa na mitazamo "hasi" kuhusu ugonjwa wa COVID-19. Kwa mfano, pale ambapo wataalamu wanasema

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

kuwa COVID-19 husambazwa kupitia mihadhara, ukuruba, na mitagusano ya watu, baadhi ya wanajamii walikuwa na mitazamo tofauti iliyo kinzani. Kauli mbili za 1 hapa chini zinashadidia mtazamo huu "hasi" wa wazungumzaji wa kikawaida kuhusu namna ugonjwa huo unavyoambukizwa.

1. *a)Utaambukizwa bila kutagusana, Korona huelea angani.*

*b) Utajizuiaje na kitu kinachoelea hewani?*

Maelezo ya kitaaluma yanaeleza kwamba, mtu akiwa katika umbali wa mita moja na nusu kutoka kwa mwenzake hawezi kuambukizwa virusi vya Korona. Hata hivyo, mtoaji wa kauli mbili hapo juu anauliza swali la kimantiki jinsi virusi vya Korona vinavyosambazwa. Mtazamo wake ni kwamba, hata mtu awe mbali na mwingine au asiwe kwenye mhadhara, lazima ataambukizwa COVID-19. Huu ni mtazamo wa kiSkaz kwa sababu unakinzana na maelezo ya kitaaluma. Mtazamo kama huu unaonesha hali ya falsafa ya kiSkaz ambayo inasaili kujizuia na ugonjwa ambao unaelea angani – hauonekani na watu wanaambiwa wajizuie nao.

Aidha lugha ya kikawaida miongoni mwa baadhi ya WaKenya ilionesha mitazamo inayotofautiana na ile ya kitaaluma kuhusu usitawi wa ugonjwa wa COVID-19 na mazingira fulani. Ilidhihirika kwamba baadhi ya WaKenya walichukulia kuwa COVID-19 husitawi na kuwalemea watu zaidi katika maeneo ya baridi baridi kuliko yale ya joto joto. Angalia mfano 2 hapa chini.

2. *a) Korona hudhihirika zaidi kule Ulaya kwa sababu eneo hilo ni baridi.*

*b) Hapa kwetu Afrika kuna joto jingi kwa sababu kuna jua kila wakati.*

*c) Korona huyeyushwa na joto.*

Lugha ya kikawaida pia ilidhihirisha kuwa, baadhi ya WaKenya huchukulia kuwa, ugonjwa wa Korona huwalemea wazungu zaidi kuliko Waafrika. Uchunguzi ulionesha kuwa, mtazamo huu ulitokana na uwingi wa vifo vilivyoripotiwa kutokea katika mataifa ya kimagharibi. Kauli 3 hapa chini inadhihirisha mwelekeo huu hasi.

3. *a) Mwafrika ana kinga thabiti kuliko mzungu. Mwafrika hawezwi na Korona.*

*b) Mwili wa Mzungu ni dhaifu, haustahimili Korona*

Kauli hizi zinadhihirisha mitazamo "hasi" kwani hakuna ushahidi wa kitaaluma unaoonesha kuwa mwili wa Mwafrika una umadhubuti au nguvu zaidi kuliko ule wa mzungu na hivyo kutoathiriwa na virusi vya Korona.

Baadhi ya mitazamo ilichangia kuibuka na kuimarika kwa unyanyapaa ulioelekezwa kwa WaKenya na WaKenya wenzao. Mathalani, wenye magari ya kibinafsi walikataa kuwabeba walioomba 'lifti' au kubebwa kwa kulipa nauli kwa kuwashuku kuwa na Korona na hivyo kuhofia kuambukizwa. Kauli 4 hapa chini inashadidia hali hii.

4. *a) Siwezi kumpa lifti, pengine ana Korona*

*b) Kumbeba ni kujitafutia Korona*

**Mitazamo Kuhusu Dalili za COVID-19**

Kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni (2020) na Wizara ya Afya nchini Kenya (2020), dalili za kawaida za ugonjwa wa COVID-19 ni kama vile: joto jingi mwilini, kukohoa, kuumwa na kichwa na kwenda chafya. Dalili hizi pia zinaweza kuashiria uwepo wa magonjwa mengine kama vile kifua kikuu, na malaria.

Ingawa mtu anaweza kuonyesha dalili hizi kuashiria kuugua magonjwa mengine mbali na COVID-19, baadhi ya wanajamii katika kipindi hicho cha tangaavu walichukulia kuwa, yeyote aliyeonyesha dalili hizi alikuwa na COVID-19. Huu ulikwa mtazamo "hasi" kwani huenda ikawa mtu anaugua magonjwa mengine. Kutokana na mtazamo huu, waliokohoa, kwenda chafya na hata kuonyesha dalili za kuumwa na kichwa hadharani waliangaliwa kwa jicho la shaka. Visa kama vile abiria kutoroka kwenye magari ya umma mtu alipokohoa au kupiga chafya sana viliripotiwa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

katika mitandao ya kijamii kama vile Whatsapp. Kwa mfano, kuna kisa ambapo abiria mmoja alizimia ndani ya matatu na badala ya abiria wenzake kumpa huduma ya kwanza, wote walitoroka na kumwacha peke yake kwenye gari.

Pamoja na hayo, mtu alipoonyesha dalili zilizotajwa hapo juu, wanajamii katika mazungumzo yao ya kawaida wangefanya utani na mhusika kama kauli nambari 5 hapa chini zinavyoonesha:

5. *a) Ama una Korona?*

*b) Vaa maski wewe!*

*c) Usituletee Korona wewe!*

*d) Usitukaribie na Korona.*

Isitoshe, wazungumzaji wa kiSkaz wangesikika wakiongea kuwahusu wengine kwa namna ya kuonesha kuwashuku kuwa na virusi vya COVID-19 hususan baada ya kuonesha dalili tulizotaja awali. Mifano ya kauli hizo za kikawaida ni hii hapa kauli 6.

6. *a) Huyu(o) ana Korona*

*b) Pengine ana Korona*

**Mitazamo kuhusu Chanjo Dhidi ya COVID-19**

Kupatikana kwa chanjo dhidi ya COVID-19 kulileta afueni kubwa kote duniani. Hii ni kwa sababu chanjo hii ilipunguza vifo vilivyosababishwa na tangaavu hilo kwa kiwango kikubwa sana na ilikuwa faafu kwa kila mtu: watoto, vijana na wazee. Hata hivyo, kutokana na mazungumzo ya kikawaida miongni mwa watafitiwa, ilibainika kuwa baadhi ya WaKenya hususan wazee walikuwa na mitazamo "hasi" kuhusiana na chanjo hii. Kauli 7 inathibitisha mtazamo huu.

7. *a) Hata sisi tunachanjwa?*

*b) Wa kuchanjwa ni watoto, sio wazee*

*c) Chanjo haiwasaidii wazee*

Kauli zilizotolewa hapo juu, ambazo zilitokana na mazungumzo ya kikwaida miongoni mwa wazee zinashereheshea mitazamo yao ya chanjo dhidi ya COVID-19. Kutokana na kauli hizi, inadhihirika kwamba, wazee waliamini kwamba chanjo haingewasaidia kitu mintaarafu ya umri wao. Aidha, waliamini kwamba chanjo, kimazoea yao, huwa ya watoto na wala si ya watu wazima, zaidi wazee. Mintaarafu ya mtazamo huu, wazee wengi hawakukimbilia kupata chanjo.

Baadhi ya WaKenya, hususan wale ambao bado wanazaa nao walidhihirisha mitazamo yao dhidi ya chanjo ya COVID-19 katika mazungumzo yao ya kiSkaz. Walifanya hivyo hasa kwa kuihusisha chanjo na suala zima la uzazi kama inavyooneshwa na kauli 8 hapa chini.

8. *a) Chanjo hupunguza nguvu za uzazi*

*b) Chanjo ni dawa ya kupanga uzazi*

Mbali na mtazamo kwamba chanjo dhidi ya COVID-19 ilikuwa njia ya kupanga uzazi miongoni mwa WaAfrika, mtazamo mwingine ulikuwa kwamba, chanjo hii ingewafanya vizazi vya baadaye vya waliochanjwa kuwa na akili punguani. Aidha, wengine waliamini kuwa chanjo hii ilikuwa silaha ya kuwaua WaAfrika kwani kutokana na mazungumzo yao ya kikawaida, mtu aliyechanjwa angekufa baada ya miaka mitatu kama invyooneshwa na kauli 9. Kimsingi, chanjo dhidi ya Korona ilionekana kama njia ya kuvuruga na hata kuua uzazi. Kutokana na mitazamo kama hii, kuna wananchi, haswa wazee ambao hawakuchanjwa mpaka wa leo, wasailiwa wengine waliarifu.

9. *a) Chanjo itafanya vizazi vijavyo kuwa na akili punguani.*

*b) Ni dawa ya kuwaua WaAfrika.*

*c) Mtu akichanjwa atakufa baada ya miaka mitatu.*

**Mitazamo kuhusu Kutafuta Huduma Hospitalini**

Kama ilivyo desturi, watu walio na magonjwa kama vile Virusi vya Ukimwi, Shinikizo la Damu,

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

Kisukari na mengineyo huwa na miadi ya kutembelea hospitali kwa nyakati mbalimbali ili kupata tiba, ushauri na nasaha. Aidha kina mama waja wazito na wale wanaonyonyesha watoto hutembelea kliniki hospitalini kwa ajili ya kupata chanjo dhidi ya magonjwa yanayowakumba watoto wachanga. Aidha, huduma nyingine zinazotolewa katika kliniki hizi ni ushauri kuhusu lishe bora namna ya kuzuia maambukizi ya magonjwa mengineyo. Huduma hizi hutolewa nyakati maalumu zilizotengewa wanaohusika.

Baada ya kuzuka kwa tangaavu la Korona, baadhi ya wateja waliotajwa hapo juu walisitisha safari zao za kutafuta huduma hospitalini kutokana na mielekeo hasi kuhusu maambukizi ya Korona. Baadhi yao walichukulia kuwa, kwenda kutafuta huduma za kawaida ni kujipeleka kwa Korona. Mawazo haya "hasi" yalibainika kupitia mazungumzo ya kikawaida ya wahusika. Mathalani, mmoja wao alisikika akisema;

10. *a) Mimi nimekosa kwenda kliniki miezi mitatu sasa.*

*b) Mwenzake alipomuuliza, kwa nini?*

*c) Aljibu, "Sitaki kwenda kuleta Korona."*

Kauli kama hizi zilizotolewa kama mifano hapo juu zinadhihirisha mitazamo "hasi" ya wanajamii kuhusu ugonjwa wa Korona kwa kuhusisha maambukizi yake na mazingira ya hospitalini. Mtazamo kama huu, licha ya kutokuwa na mashiko shadidi ulisababisha madhara zaidi kuliko madhara yaliyoletwa na Korona. Hii ni kwa sababu wengi waliathirika na magonjwa yao ya kawaida kwa kuutoroka Korona.

**Mtazamo kuhusu Unawaji Mikono**

Kunawa mara kwa mara mikono kwa kutumia sabuni ni mojawapo ya mikakati ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya Korona na ulitiliwa nguvu. Hata hivyo, utafiti huu ulibainisha kuwa, kupitia kwa mazungumza ya kikawaida, wananchi walichukulia mkakati huu kimzaha na hivyo kudhihirisha mwelekeo "hasi" dhidi ya mkakati wenyewe. Mazungumzo kati ya Mtu I na Mtu II katika kauli 11 hapa chini yanashadidia mtazamo huu hasi.

11. *Mtu wa I: Eeee, usiingie kibandani mwangu bila kunawa mikono*

*Mtu wa II: Kuna chakula?*

*Mtu wa I: Aaa, si ni Korona*

*Mtu wa II: Hatuli Korona*

*Mtu wa I: Wacha zako, nawa, usiniletee*

*Mtu wa II: Haki, hii Korona ni noma. Tumezoea kunawa kabla ya kula, sasa twanawa bila kula*

Mintarafu ya mfano wa mazungumzo ya kikawaida tuliyotoa hapo juu, ni dhahiri kwamba, wazungumzaji wanaweza kuingiza mzaha kwenye jambo zito linalowakabili kama hili janga la COVID-19. Kwa kufanya hivyo wameweza kupuuza fikira za kitaalamu kuhusu unawaji mikono na pia kuleta dhihaka ili kupunguza ukali wa umuhimu wa kupambana na tangaavu hilo.

**HITIMISHO**

Utafiti huu umedhihirisha na kujadili mitazamo hasi kuhusu tangaavu la COVID-19 miongoni mwa baadhi ya WaKenya. Mitazamo hii imedhihirika kupitia mazungumzo ya kikawaida, yaani Skaz. Mitazamo hii imeonesha mwonoulimwengu wa watafitiwa kuhusiana na janga la COVID-19. Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yameweka wazi umuhimu au mchango wa masemezano ya kiSkaz kwa taaluma ya afya. Hii ni kwa sababu, wataalamu wa kiafya wanaona masimulizi ya kiSkaz kuwa ya 'upotoshi' na ndiposa huibua maelekezo yanayolenga kurakibisha 'upotoshi' huu. Mbali na kuuliza maswali ya kimantiki ya mtu asiye msomi wa tiba, kuendeleza kaulitaasubi, kauli za hofu na unyanyapaa, kauli za kutojali, na kauli za mzaha imetudhihirikia kuwa kauli hizi hazikutolewa kwa makusudi ya kudanganya na hivo kupotosha kauli za wataalamu wa afya bali ilikuwa ni mwonoulimwengu wa makabwela ambao hawakubali kufungwa na mipaka ya sheria katika uzungumzaji wao kama invyojitokeza katika

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1754

Mbinu ya Urazini wa Kiwatu. Kwa hivyo, utafiti huu umeonesha kuwa, masimulizi ya kiSkaz yawe msingi mmojawapo wa maelekezo au fatwa za kitaaluma zinazotolewa na wataalamu wa afya katika kupambana na majanga tangaavu.

**MAREJELEO**


AFP. (2020) Covid Pandemic and Lockdown: How 2020 Changed the World. Ilisomwa https://www.standardmedia.co.ke/article/2001398421/covid-pandemic-and-lockdown-how-2020-changed-the-world

Bakhtin, M.M (1981). Dialogic Imagination: Four essays. Michael H. (mh). Texas University Press.

BBC (8 June, 2020) Coronavirus: John Magufuli declares Tanzania free of Covid-19. Ilisomwa: https://www.bbc.com/news/world-africa-52966016

CGTN. (24 August, 2020). Misconceptions on COVID-19 persists in Kenya's rural areas. Ilisomwa: https://newsaf.cgtn.com/news/2020-08-24/Misconceptions-on-COVID-19-persists-in-Kenya-s-rural-areas-Te1cCee03m/index.html

Kilonzo, S.M na Omwalo, B.O. (2020). The politics of pulpit reliogiosity in the era of COVID-19 in Kenya. Ilisomwa: https://www.frontiersin.org/articles/10.3389/fcomm.2021.616288/full

Mghenyi, C. (7 May, 2020). Is Joho a hero or a villain in the fight against Covid-19? Ilisomwa: https://www.the- star.co.ke/news/big-read/2020-05-07-is-joho-a-hero-or-a-villain-in-the-fight-against-covid-19/

Mghenyi, C. (24 May, 2020). Mombasa slums flirt with Covid-19 explosion. Ilisomwa: https://www.the- star.co.ke/news/big- read/2020-05-24-mombasa-slums-flirt-with-covid-19-explosion/

Ministry of Health (2020). Frequently asked questions about Coronavirus (COVID-2019). Republic of Kenya.

Ozili, P.K na Arun, T. (2020) Spillover of COVID-19: Impact on the Global Economy. https://papers.ssrn.com/sol3/papers.cfm?abstract_id=3562570

Reliefweb (2020). Kenya Situation Report, 14 May 2020. Ilisomwa: https://reliefweb.int/report/kenya/kenya-situation-report-14-may-2020

Sacks, H., Schegloff, E.A., and Jefferson, G. (1974). A simplest systematics for the organization of turn-taking in conversation. Katika *Language 50*, 696-735.

Schmid, Wolf: "Skaz". In: Hühn, Peter et al. (eds.). *The living handbook of narratology*. Hamburg University. URL = http://www.lhn.unihamburg.de/article/skaz [Ilisomwa:12 Feb 2021]

Vidija, P. (2021). Facts or myths?: Demystifying Covid- 19. Ilisomwa https://www.standardmedia.co.ke/fact- check/article/2001416708/facts-or-myths-demystifying-covid-19

World Health Organization (2020). Advice for public myth usters. https://www.who.int/emergencies/diseases/novel- coronavirus- 2019/advice- for- public/myth- busters?gclid=EAIaIQobChMI_Z6t_8n2_AIVwuDtCh02WQ1HEAAYASACEgKq9fD_BwE


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.